# ALLAH (S.W) HAJAFANANA NA KITU

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

ALLAH (S.W) HAJAFANANA NA KITU

-:Miongoni mwa sifa nyengine za Allah (s.w) ni

.MWENYEEZI MUNGU SI KIUMBE, HANA KIWILIWILI NA KATU HAONEKANI

Sisi tuna imani ya kuwa; Mwenyeezi Mungu haonekani kwa macho katu, kwa sababu kuona kwa macho kunamaanisha kuwa Mwenyeezi Mungu ni kiumbe aliye na kiwiliwili, aliye katika sehemu maalumu, au umbo maalumu, hali ya kwamba sifa hizoo ni sifa za viumbe vilivyoumbwa na Mwenyeezi Mungu, hali ya kwamba ubora na utukfu wa sifa za Mwenyeezi Mungu uko juu zaidi, kiasi ya kwamba haiwezekani kumfananisha Yeye na sifa za viumbe, kwa hivyo hatuwezi kumsifu Mwenyeezi Mungu kwa sifa za viumbe vyake, kwa hiyo kuwa na itikadi ya kumuona Mwenyeezi Mungu sio sahihi, na itikadi hiyo ni miongoni mwa aina fulani za shirki, -:na huko ndio kumshirikisha Mwenyeezi Mungu, Mwenyeezi Mungu Mtukufu anasema

لاَّ تُدْرِكُهُ الاَبْصَارُ وَهُوَ يُدْرِكُ الاَبْصَارَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ[1]

.Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho. Naye ni Mjuzi, Mwenye khabari

Na ni kwa dalili hiyo basi, kaumu ya Bani Israili ikatoa hoja kumwambia Nabii Mussa (a.s) kuwa -:hawatamuamini Mwenyeezi Mungu isipokuwa pale watakapomuona, pale waliposema

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَي لَن نُّؤْمِنَ لَكَ حَتَّي نَرَي اللهَ جَهْرَةً فَاَخَذَتْكُمُ الصَّاعِقَةُ وَاَنتُمْ تَنظُرُونَ[2]

Na mlipo sema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumwone Mwenyezi Mungu waziwazi. .Ikakunyakueni radi nanyi mnaangalia

:Maelezo kuhusiana na Aya

.Kisa cha Mayahudi kutaka kumuona Mwenyeezi Mungu wazi wazi kinatajwa pia katika Talmud

Basi Nabii Mussa (a.s) akaipeleka kaumu hiyo katika mlima ujulikanao kwa jina la Tur, akakariri mahitajio yao na hoja zao walizozitoa za kumuona Mwenyeezi Mungu, basi Nabii Mussa (a.s) -:akasikia jawabu hii kutoka kwa Mola wake

وَلَمَّا جَاء مُوسَي لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ قَالَ رَبِّ اَرِنِی اَنظُرْ إِلَيْكَ قَالَ لَن تَرَانِی وَلَـكِنِ انظُرْ إِلَي الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ تَرَانِی فَلَمَّا تَجَلَّي رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكّاً وَخَرَّ موسَي صَعِقاً فَلَمَّا اَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ إِلَيْكَ وَاَنَاْ اَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ[3]

Na alipo kuja Musa kwenye miadi yetu, na Mola wake Mlezi akamsemeza, alisema: Mola wangu Mlezi! Nionyeshe nikutazame. Mwenyezi Mungu akasema: Hutoniona. Lakini utazame .huo mlima

Ukibaki pahala pake basi utaniona. Basi alipo jionyesha Mola Mlezi wake kwa mlima, aliufanya uvurugike, na Musa akaanguka chini amezimia. Alipo zindukana alisema: Subhanaka, !Umetakasika

.Natubu kwako, na mimi ni wa kwanza wa Waumini

.Ni tukio hilo basi ndilo lililothibitisha kuwa Mwenyeezi Mungu haonekani katu

Sisi tuna itikadi ya kuwa; ikiwa kuna baadhi ya Aya na Riwaya za Kiislamu zinaelezea kuhusu kuonekana kwa Mwenyeezi Mungu, makusudio ya Aya hizo sio kuonekana kwa macho, bali ni kuonekana ndani ya nyoyo, na kushuhudiwa ndani ya nafsi za wanaadamu. kwa sababu siku .zote Aya za Qur-ani zinazifasiri Aya nyengine

القران يفسر بعضه بعضا[4]

.Kwa hakika Qur-ani inafasiri baadhi ya Aya nyengine

Mbali ya hayo, tukiongezea kuithibitisha kauli hiyo, Imamu Aliy (a.s) alipokuwa akijibu suala la :mmoja wa wafuasi wake, pale alipoulizwa

يا امير المؤمنين هل رأيت ربک.

yaani, Ewe Amiyrul-Muuminiyna, hivi kweli umewahi kumuona Mola wako? Imamu Aliy (a.s) yaani, hivi kweli nitaabudu nisiyemuona?. baadae ; أأعبـــد مـــالا ارى :akamjibu kwa kumwambia -:akaendelea kwa kusema

" لا تدركه العيون بمشاهدة العيان. ولكن تدركه القلوب بحقايق الايمان[5] "

Macho katu hayawezi kumuona Mwenyeezi Mungu kwa uwazi, lakini nyoyo na nafsi za wanaadamu kwa kutumia nguvu za imani zinaweza kumuona Allah (s.w).

Sisi tuna itikadi ya kuwa; Kumnasibisha Mwenyeezi Mungu kwa sifa za viumbe, kama mwenyeezi Mungu kuwa na sehemu au zama maalumu, kuwa ana kiwiliwili, au kuwa na itikadi ya kuwa Mwenyeezi Mungu anaweza kushuhudiwa kwa macho, husababisha kuwa mbali na taaluma au elimu ya kumtambua Mwenyeezi Mungu, na mwenye na itikadi hizo basi atakuwa amemshirikisha Mwenyeezi Mungu, ndio Mwenyeezi Mungu (s.w) ni mbora wa kila kitu, na mbora wa kila sifa, na hakuna kitu chochote kinachofanana na Yeye.[4] Hiyo ni hadithi maarufu iliyonukuliwa na Ibni Abbasi, lakini vile vile hadithi hiyo imenukuliwa kwa mtindo mwengine na Amiyrul-Muuminina Imamu Ali (a.s) ndani ya kitabu chake cha Nahjulbalagha, ان الكتـــاب يصـــدق بعضـــه بعضـــا... yaani kwa hakika Qur-ani inafasiri baadhi ya aya nyengine. (Nahjulbalagha, hutuba ya 18), na katika riwaya nyengine, imekuja kwa mtindo huu وينطـــــق بعضه ببعض ويشهد بعضه على بعض.

yaani kwa hakika Qur-ani inabainisha baadhi ya aya, na inabainisha na kutoa shahada ya baadhi za Aya. (Nahjulbalagha, hutuba ya 103.)

[1] Surat Al-An-aam Aya ya 103

[2] Suratul-Baqarah Aya ya 55

[3] Surat Al-Aarafu Aya ya 143.

[5] Nahjulbalagha, hutuba ya 179.

MWISHO